# DARASA LA NANE

# SIGNAL EXAMS 2020

DIGITAL EDITION
021

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA:
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.

9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.
   **Mfano**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

**21.** Doa ni kwa dosari kama ilivyo uzembe kwa:-
   A. mvivu
   B. ubwete
   C. uchoyo
   D. bidii

   Jibu sahihi ni **B (ubwete)**

**Katika karatasi ya majibu**

**1** [A] [B] [C] [D]   **11** [A] [B] [C] [D]   **21** [A] [■] [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

*© All rights reserved. No direct reprint, duplication, photocopying or sharing on social media platforms without the prior written permission of the publisher.*

**GEUZA UKURASA**

**Signal Publishers Limited**

Signal Exams   @Signalexams

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* 1 *mpaka* 15. *Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa jibu lifaalo zaidi.***

Kuvumbuliwa kwa simutamba ____1____ mawasiliano pakubwa. Maendeleo haya ya kiteknolojia ____2____ watu ____3____ watakapo bila ____4____ za wakati wala masafa. ____5____ kupigiana simu, watu hutuma ujumbe ____6____ unaoitwa ____7____. Ujumbe huu unaweza kutumwa kwa mtu mmoja au kundi la watu ____8____. Ama kweli ulimwengu ____9____ kimaendeleo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. imerahisisha | B. kumerahisisha | C. yamerahisishwa | D. kumerahisia |
| **2.** | A. yameezesha | B. imewezesha | C. kimewezesha | D. yamewezesha |
| **3.** | A. kuwasiliana | B. kuwasili | C. kuwasilisha | D. kuwasilishana |
| **4.** | A. vikwazo | B. tofauti | C. pingamizi | D. matatizo |
| **5.** | A. Fauka ya | B. Badala ya | C. Kinyume na | D. Kati ya |
| **6.** | A. fupi | B. mfupi | C. refu | D. ndefu |
| **7.** | A. mdahalishi | B. kipepesi | C. arufu | D. arafa |
| **8.** | A. sawa | B. asilani | C. sawia | D. kiholela |
| **9.** | A. umepiga hatua | B. umepiga jeki | C. umepiga misamba | D. umepiga kumbo |

Idadi kubwa ya wanafunzi ____10____ kujisomea bila msaada wa walimu. Wengi hufungua kurasa ____11____ vitabu na kutumbua macho tu bila kung'amua lolote. Baadaye wao ____12____ mitihani inapoletwa ____13____ wakijipata hawana lolote la kujivunia. ____14____; wanafunzi hawa wanapaswa kujifunza kutoka kwa walimu wao kisha waifuate ____15____ hiyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. hawajui | B. haijui | C. hamjui | D. hawakujua |
| **11.** | A. ya | B. wa | C. la | D. za |
| **12.** | A. huangamia | B. huridhika | C. huhangaika | D. hutabasamu |
| **13.** | A. huku | B. wala | C. huko | D. hapo |
| **14.** | A. Mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina | B. Ushikwapo shikamana | C. Msafiri ni aliye pwani | D. Mtu hujikuna ajipatapo |
| **15.** | A. mwelekeo | B. mielekeo | C. nyaadhi | D. kielelezo |

***Kuanzia nambari 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua orodha yenye vielezi pekee.
A. Tena, ghafla, ajabu, mno.
B. Laini, aghalabu, kiasi, tele.
C. Jepesi, polepole, sana, vigumu.
D. Tano, dhaifu, bora, safi.

**17.** Upi ni ukanusho wa:
Swali ambalo aliuliza limeweza kujibiwa.
A. Swali ambalo aliuliza halikuweza kujibiwa.
B. Swali ambalo hakuuliza halijaweza kujibiwa.
C. Swali ambalo hakuuliza halikuweza kujibiwa.
D. Swali ambalo aliuliza halijaweza kujibiwa.

**18.** Chagua wingi wa sentesi ifuatayo:
Seremala aliutumia ubao mwembamba.
A. Seremala walitumia mbao nyembamba.
B. Maseremala waliyatumia mabao membamba.
C. Seremala walizitumia mbao nyembamba.
D. Maseremala walizitumia mbao nyembamba.

**19.** Ni sentensi ipi iliyo katika wakati uliopo hali isiyodhirika?
A. Sote twajua kuogelea vizuri.
B. Washi wanabeba mawe migodini.
C. Kikombe kimeletwa na kuoshwa.
D. Ndege ingalianguka abiria wangalifariki.

**20.** Ni jibu lipi lenye maneno yasiyoambatanishwa ipasavyo?
A. Ona - Onevu.
B. Cheka - Cheshi.
C. Dhulumu - Dhalimu.
D. Kaa - Kaidi.

**21.** Tone ni kwa jasho na doti ni kwa:-
A. nguo B. leso
C. damu D. samaki.

**22.** Andika katika usemi wa taarifa
"Yawekeni madawati yenu darasani humu," mwalimu aliwaambia wanafunzi wake.
A. Mwalimu aliwaambia wanafunzi wake wayaweke madawati yao darasani humu.
B. Mwalimu aliwaambia wanafunzi wake wayaweke madawati yao darasani humo.
C. Mwalimu aliwaamuru wanafunzi wake wayaweke madawati yao darasani humo.
D. Mwalimu aliwaambia wanafunzi wako wayaweke madawati yenu darasani humo.

**23.** Kuni jikoni huanikwa kwenye:-
A. uchaga B. susu
C. bembea D. kifumbu.

**24.** Neno 'Muhtasari' lina silabi ngapi?
A. Tisa B. Nne
C. Tano D. Saba

**25.** Andika ukubwa wa sentensi ifuatayo:
Kikapu kimejaa maembe.
A. Kapu limejaa maembe.
B. Jikapu limejaa majembe.
C. Jikapu limejaa jijembe.
D. Kapu limejaa majiembe.

**26.** Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendewa.
Juma alienda kwa Muasya akalima shamba.
A. Shamba lililimiwa kwa Juma na Muasya.
B. Shamba la Muasya lililimiwa kwa Juma.
C. Juma alilimiwa shamba na Muasya.
D. Muasya alilimiwa shamba na Juma.

**27.** Tegua kitendawili kifuatacho.
Anatafuna lakini hamezi.
A. Shoka. B. Ulimi.
C. Ng'ombe. D. kivuli.

**28.** Fuma ni kutengeneza kitu kwa kusokota nyuzi. Fuma aidha ni:-
A. kitu kilichoviringwa
B. mtu aliyejeruhiwa kwa mkuki
C. toka kwa maji ufukoni na kwenda sehemu ya mbali ya bahari
D. Mkuki wenye chembe kipana

**29.** Tajiri akiharibikiwa au akifilisika hawezi kukosa akiba japo ndogo
Chagua methali inayolingana na maelezo haya.
A. Kutoa ni moyo usambe ni utajiri.
B. Jungu kuu halikosi ukoko.
C. Chururu si ndo ndo ndo!
D. Hakuna ziada mbovu.

**30.** Bainisha kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:
Mto huu ni salama lakini ule una mamba wengi sana.
A. Huu B. Ule
C. Salama D. Lakini

***Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia 31 hadi 40.***

Tenge alisikia kondakta akiitwa Ringo na dereva. Kondakta alipoanza kukusanya nauli alimpita Tenge makusudi, ingawa Tenge alimnyoshea mkono kumpa nauli yake. Jambo la kustaajabisha ni kwamba Ringo alimwambia Tenge apoe tu, leo angemlipia. Tenge alifurahi sana kuona kuwa siku hiyo ilikuwa ya bahati kwake, kwani hakuokoa shilingi hamsini tu bali alipata rafiki mpya. Aliwaza moyoni mwake", kumbe makondakta si ibilisi kama wanavyochukuliwa?"

Tenge alipofika mjini alishuka na **kushika hamsini zake** za kuabiri basi jingine na kuendelea na safari ya shule. Alikuwa msichana wa darasa la nane katika shule ya mchana iliyokuwa ng'ambo ya pili ya mji.

Baada ya juma moja Tenge alibahatika tena kuiona matau ile tena katika kituo cha mabasi. Safari hii hakusita kamwe bali aliiabiri moja kwa moja na kumwamkia kondakta. Alikuwa ni yule yule kijana mtanashati kwa jina Ringo. Matatu haikuwa na watu wengi na Ringo alipata wasaa wa kumtupia Tenge maneno mawili matatu tena kwa kiingereza. Tenge alistaajabu kwamba alikuwa amesoma. Wakaanza usuhuba, ikawa ni kawaida kwa Tenge kusafiri bure katika matatu hiyo.

Siku moja Ringo alimwalika Tenge kwa matembezi katika safari zao za matatu. Siku hiyo Tenge alibeba nguo za kubadilisha katika shanta yake. Baada ya kufika mwisho wa safari ya kwanza ya matatu, Tenge alipewa nafasi ya kubadilisha nguo zake. Dereva akalipeleka gari mahali penye faragha; yaani kwenye barabara isiyo na magari mengi. Ringo alianza kumwonyesha Tenge zawadi fulani alizomnunulia. Tenge kuona hivyo aliduwaa na kumtazama Ringo kwa uso wa shukrani.

Baada ya mwezi mmoja wa matukio haya katika maisha ya Tenge, masomo yake yalianza kuzorota. Alikuwa hatilii maanani sana. Hata walimu walianza kumdadisi. Siku alizokuwa akienda matembezini na Ringo, alizoea kudanganya kwamba alikuwa mwele. Siku moja Tenge alimwambia Ringo tatizo la masomo yake. Hapo ndipo Ringo alipomwambia kwamba angeweza kumsaidia kutatua shida hiyo. Walipanga matembezi mengine ili Ringo amweleze Tenge suluhisho hilo.

Kesho yake **walikutana kama ilivyokuwa ada yao faraghani**. Tenge alikuwa na hamu sana ya kujua jibu hili. Alikuwa hataki kumkosea Ringo pamoja na kuwahuzunisha wavyele wake kwa kuacha shule. Ringo alimweleza kwamba alikuwa na kitu ambacho kingemsaidia kufanya vyema katika masomo yake.

Ndipo alipomtolea Tenge aina ya sigara na kumweleza kwamba sigara hiyo ilikuwa na dawa iliyochangamsha ubongo. Tenge hakutafakari dawa hiyo ilikuwa nini na ilichangamsha ubongo vipi! Yeye alitaka tu suluhisho la tatizo lake. Alingojea kupewa masharti yanayoambatana na sigara hiyo.

Tenge hakuwa amewahi kuvuta sigara tena, hakupendelea wanawake walio na hulka hiyo. Moyoni aliwaza ikiwa nitaivuta katika siri tena mara moja kama dawa na itanisaidia, haina neno!" Alipoonyeshwa jinsi ya kuivuta sigara hiyo aliichukua na kujaribu. Mara ya kwanza moshi ulizua kukohoa na machozi nayo yalimtiririka. Alihisi kama kifua kinapasuka. Kumbe chombo chake kilikuwa kimeenda mrama na sasa kilielekea kuzama!

**31.** Kulingana na aya ya kwanza:-
A. Ringo aliamua kumpuuza Tenge
B. Tenge hakutaka kulipa nauli yake
C. Ringo alimpita Tenge makusudi
D. Tenge hakuwa na pesa za nauli.

**32.** Chagua kauli iliyo sahihi.
A. Nauli ya kuenda shuleni ilikuwa shilingi hamsini.
B. Makondakta wengi walikuwa na sifa mbovu
C. Ringo na Tenge walikuwa wamekutana awali
D. Matwana ilimbeba Tenge kutoka mjini.

**33.** **Alishuka na kushika hamsini zake,** maana yake ni kuwa:-
A. alishuka na kushika shilingi zake hamsini
B. alishuka baada ya kulipa shilingi hamsini
C. alishuka na kukimbilia shuleni
D. alishuka na kujiendea kwenye shughuli zake.

**34.** Shule ya akina Tenge ilikuwa ya:-
A. kutwa
B. mseto
C. bweni
D. upili.

**35.** Lililomshangaza Tenge ni kung'amua:-
A. kuwa Ringo na dereva walikuwa wasomi
B. kuwa Ringo angeweza kuongea kimombo
C. kuwa Ringo angempeleka matembezini
D. kuwa makodakta walikuwa matembezini.

**36.** Tenge alizipataje nguo za kubadilisha?
A. Aliletewa na Ringo kwenye matwana.
B. Aliondoka nyumbani bila kuvalia sare.
C. Alizibeba kwenye mfuko wake wa vitabu.
D. Alizivalia ndani ya sare yake.

**37.** Madhara yaliyoletwa na uhusiano wa Ringo na Tenge ni :-
A. Tenge kuwa mwele na masomo kuzorota
B. Tenge kupewa zawadi na masomo kuzorota
C. Tenge kubugia vileo na kutofika shuleni tena
D. Tenge kukosa makini na masomo kuzorota.

**38.** Walimu walikuwa wawajibikaji kwa kuwa:-
A. waliweza kulitambua tatizo la Tenge
B. walisaili chanzo cha masomo kuzorota
C. walimshauri Tenge kuhusu mienendo yake
D. walimwomba Tenge azingatie masomo yake.

**39.** "....walikutana kama ilivyokuwa ada yao faraghani yaani:-
A. walikutana faraghani kama walivyoahidiana
B. walikutana kwenye matatu kama walivyozoea
C. walipatana asubuhi Tenge akienda shuleni
D. walikutana pembeni kama walivyozoea.

**40.** Kulingana na aya ya mwisho:-
A. matatizo ya Tenge yangezidi kuongezeka
B. sigara ilichangamsha ubongo wa Tenge
C. Tenge hakujua kuwa sigara ina madhara
D. wazazi walimsihi Tenge asiache shule.

***<u>Soma kisa kifuatacho  kisha ujibu maswali</u>***  **<u>41 *hadi* 50.</u>**

Kila siku niamkapo, mimi hufikiria kuhusu mtafaruku unaohusiana na maisha yetu. “Ni jukumu la serikali,” wengi huishia kusema kuhusiana na matatizo yanayokumba jamii yetu. “Serikali inahitaji kulishughulikia tatizo hili kwa haraka,” wengine husema ilhali wengine hulalama **wakinong’onezana**, “Serikali lazima ijitolee mhanga kuboresha hali ya watu wake, au sivyo....”

Serikali ni wewe. Serikali kumbe ni mimi. Serikali si dude. Mtazamo wetu finyu umetufanya kujitwika mzigo mzito usio wetu huku tukipiga kelele zisizoisha na zisizo na maana.

Jukumu ni letu. Lazima **kila mmoja wetu kuchukulia kuwa tatizo lililo miongoni mwetu linaweza kutatuliwa na mimi na wewe**. Hebu fikiria kidogo. Wewe kama mwanafunzi ikiwa ungemwachia huyo dude unayemwita serikali kila kilicho chako kukutekelezea ingekuwaje?

Kama ungedai kuwa serikali inafaa kusoma kwa niaba yako ili wewe ule matunda tu! Kama ungekataa kufanya kazi yako uliyopewa na mwalimu darasani. Kwa kuwa ni jukumu la serikali kuhakikisha wanafunzi hawasumbuliwi na walimu. Ama kama ungekataa kumheshimu mwalimu wako kwa kuwa ni haki yako kutomheshimu.

Ama tuangalie suala hili kwa mapana zaidi. Hebu fikiria kama kila mtu angetupa ganda la ndizi popote alapo ama karatasi kwa sababu ni jukumu la serikali kuokota uchafu huo? Au jamaa kujichukulia sheria mkononi mwao na kuanza kulishana makonde wanapokasirika kwa sababu polisi wapo kuhakikisha kuwa utangamano upo miongoni mwetu! Hali ingekuwaje?

Kwanza ni jukumu la kila mmoja wetu kupiga kelele kuhusiana na uovu katika mazingira yetu  kunyamaa kuna balaa yake, maangamizi ya milele! Piga kelele na umwambie mwenzako, majirani na marafiki wakusaidie kufanya hivyo. Utashangaa, mwizi atatoroka, uovu utaondoka.

Pili kuna haja kukaa ange katika yale yote yanayotendeka miongoni mwetu. Kuwa macho kutasaidia kujua yanayokwenda mrama na kusaidia kuyarekebisha. Tuwajibike katika kushughulikia matatizo tuliyo nayo. Mwito wetu unafaa kuwa. “Hakuna mwingine mimi ndimi!” Kuwa na mtazamo kama huu kutasaidia kuondoa siri kubwa iliyo katika serikali.

**41.** Mwandishi anasema kuwa:-
A. maisha yake yamejaa mitafaruku
B. amekata tamaa kuhusu maisha ya jamii
C. wote hufikiria kuhusu fujo za maisha
D. kila siku hujipata akiwazia migogoro ya maisha.

**42.** Maana ya "**wakinong'onezana**" ni:-
A wakidanganyana
B. wakiambiana waziwazi
C. wakiongea kwa sauti za chini
D. wakilaumiana.

**43.** Watu wanaorejelewa katika aya ya kwanza ni:-
A. wazalendo
B. walegevu
C. walowezi
D. waona mbele.

**44.** Mwandishi anaonelea kuwa serikali ni
A. kila anayewajibika
B. Rais na viongozi
C. watu wengine wote
D. dude lisilojulikana.

**45.** **Lazima kila mmoja wetu kuchukulia kuwa tatizo lililo miongoni mwetu linaweza kutatuliwa na mimi na wewe.**
Ni methali gani inayolingana na kauli hii?
A. Manahodha wengi chombo huenda mrama.
B. Nia zikiwa moja kilicho mbali huja.
C. Kilio huanza mfiwa ndipo wa mbali wakafuata.
D. Maji ya kifuu ni bahari ya chungu.

**46.** Mwanafunzi hawezi kuiachia serikali majukumu yake kwa kuwa:-
A. haiwezekani kufanya hivyo
B. ataadhibiwa na walimu wake
C. atakosa kufaulu maishani
D. atalaumiwa na wazazi wake.

**47.** Aya ya tano inapinga:-
A. kuiachia serikali majukumu muhimu
B. utupaji wa maganda ya ndizi
C. kuiachia serikali kuokota uchafu
D. kulipiza kisasi baada ya kukosewa

**48.** Kujichukulia sheria mikononi mwao ni:-
A. kupigana bila sababu yoyote.
B. kutekeleza majukumu yanayotengewa serikali
C. kujaribu kukomesha dhuluma
D. kulipiza kisasi baada ya kukosewa.

**49.** Maoni ya mwandishi ni kuwa:-
A. kila mmoja akiwajibika maovu yataangamizwa
B. nguvu za kumaliza uhalifu zote ni za raia
C. wezi wote hutoroka wanapopigiwa kelele
D. kupiga kelele huangamiza maovu yote

**50.** Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni:
A. Jukumu la serikali.
B. Maovu ya kijamii.
C. Wajibu wa mzalendo.
D. Hakuna mwingine, wewe ndiwe.